UTANGULIZI WA

ELIMU YA KUITETEA IMANI

MAJIBU YA MITIHANI

shepherds
GLOBAL CLASSROOM

UTANGULIZI WA ELIMU YA KUITETEA IMANI

MAJIBU YA MASWALI YA MAJARIBIO

shepherds
GLOBAL CLASSROOM

Somo la 1
Utangulizi wa Elimu ya Kuitetea Imani

(1) Je, ni nini ufafanuzi wa Elimu ya kuitetea imani ya Kikristo?

Elimu ya kuitetea imani ya Kikristo ni kuwasilisha ushahidi unaothibitisha ukweli wa Imani ya Kikristo.

(2) Kwa nini tunasema elimu ya kuitetea Injili ni muhimu wakati wa kufanya Uinjilisti?

Watu wengi huja kwa Kristo baada ya kujifunza ushahidi wa ukweli uliopo kuhusiana na Ukristo.

(3) Kwa nini tunasema elimu ya kuitetea imani ni muhimu baada ya Uinjilisti?

Kujua ni kwa nini umeamini kutakufanya uwe na nguvu katika imani ya Kikristo.

(4) Ni aya gani katika Agano Jipya inayoonyesha kwamba kuna hitaji la kutumia elimu ya kuitetea imani? Inukuu aya hiyo.

1 Petro 3:15 "Bali mtakaseni Kristo Bwana mioyoni mwenu, mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu."

(5) Kuna maswali mangapi yanayoulizwa kuhusu elimu ya kuitetea imani katika 1 Petro 3:15?

Swali la 1: Kuna haja yeyote ya kutumia elimu ya kuitetea imani?
Jibu la 1: Ndiyo, Wakristo wanapaswa wakati wote wawe tayari kutoa utetezi na maelezo yenye sababu za sisi kuwa na imani ya Kikristo.

Swali la 2: Tuwafikie nani kwa elimu ya kuitetea imani?
Jibu la 2: Mtu yeyote anayehoji sababu za sisi kuwa na imani ya Kikristo.

Swali la 3: Tuiwasilisheje elimu ya kuitetea imani?
Jibu la 3: Kwa upole na heshima.

(6) Unapokuwa unashirikisha wengine imani yako, ni kipi kianze kwanza, injili au elimu ya kuitetea imani? Kwa nini?

Katika hali nyingi wasilisha injili kwanza kwa sababu ndio ujumbe muhimu.

(7) Kuna sababu ngapi tatu za watu kuukataa Ukristo?

- Ujinga
- Kiburi
- Matatizo ya maadili

(8) Kwa nini ni lazima tujibu upinzani wa kiakili hata kwa watu ambao wana sababu za ndani kabisa za kutoamini?

Watu hawa wanaweza kuhitaji majibu ya upinzani wao wa kiakili kabla hawajatambua sababu zao za kumkataa Kristo.

(9) Ni mtu gani anayefungua macho ya wale ambao kiroho ni vipofu?

Mungu

(10) Ni kwa jinsi gani Roho Mtakatifu anaitumia elimu ya kuitetea imani kuwaleta watu kwenye imani katika Kristo?

Mungu hutumia maelezo yaliyoko kwenye elimu ya kuitetea imani katika kusaidia kufungua macho ya wale ambao ni vipofu wa kiroho.

(11) Inamaanisha nini kwa kusema kwamba maandiko yanajithibitisha yenyewe?

Kwa kuwa Biblia ni Neno la Mungu, inasema na mioyo yetu kuhusu ukweli wake.

(12) Orodhesha mambo manne ambayo Mungu huyatumia kuudhirisha utukufu wake kwenye macho ya kiroho ya moyo.

- Kupitia uumbaji
- Katika ubinadamu na kujitoa sadaka kwa Yesu Kristo
- Kupitia injili
- Kupitia maisha na shuhuda za walioamini

Somo la 2
Dhana potofu dhidi ya Elimu ya Kuitetea Imani

(1) Ni mambo gani muhimu yanayohusika na njia ya kisayansi?

- Mazingira yaliyodhibitiwa
- Majaribio ya kurudia rudia tena na tena

(2) Badala ya njia ya kisayansi, matukio ya kihistoria yathibitishwe kwa njia gani?

Njia ya sheria-historia ya kuthibisha.

(3) Kuna aina ngapi tatu za ushahidi katika ushahidi unaoutumika kuthibitisha njia ya sheria-historia?

- Ushahidi ulioandikwa
- Ushahidi wa kusimuliwa kwa mdomo
- Ushahidi halisi wa kuona kwa macho

(4) Kwa nini tunasema, "Hatuwezi kuthibitisha tukio lolote la kihistoria kwa uhakika wa asilimia 100%"?

Kwa sababu tukio lililotokea zamani sisi hatukuwepo

(5) Kama huwezi kuthibitisha kitu kwa uhakika kabisa, lakini unao uthibitisho wa kutosha wa kuweza kuleta imani ya ndani kabisa kwamba ni kweli (na uko tayari kuishi sawa na imani hiyo ya ndani), wewe una **hakika wa kimaadili**.

(6) Kauli ya kila ukweli siyo lazima uwe kweli **inajichanganya yenyewe**, hivyo haiwezekani kuwa kweli.

(7) Ukweli ni nini?

Ukweli ni wazo au maelezo yanayoendana na uhalisia.

(8) Haitoshi tu kuamini. Ni lazima tuiweke imani yetu kwa usahihi katika **Kitu Fulani**.

(9) Orodhesha dhana nne potofu dhidi ya elimu ya kuitetea imani zilizofundishwa katika somo hili. Toa majibu mafupi kuhusiana na kila dhana.

Dhana potofu ya 1: Ukristo ni lazima uthibitishwe kwa njia ya Kisayansi.
Jibu la 1: Matukio ya kihistoria, huthibitishwa kwa njia ya sheria-historia.

Dhana potofu ya 2: Ukristo ni lazima uthibitishwe kwa asilimia 100% ya uhakika
Jibu la 2: Huwezi ukathibitisha tukio lolote la kihistoria kwa uhakika wa asilimia 100%. Linathibitishwa na uhakika wa maadili.

Dhana potofu ya 3: Kila mtu ana ukweli wake binafsi
Jibu la 3: Kauli hii inajichanganya yenyewe.

Dhana potofu ya 4: Uaminifu ni Muhimu kuliko Ukweli
Jibu la 4: Ni kitu tunachoamini, na wala siyo imani peke yake inayoweza kuokoa.

(10) Nukuu kutoka kichwani 2 Wakorintho 10:4-5.

> "Maana silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome; tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu; na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo."

Somo la 3
Je, Mungu Yupo?

(1) Ni swali gani linaloulizwa na Hoja ya Kosmolojia?

Kwanini dunia ipo?

(2) Ni kwa jinsi gani Hoja hii ya Kosmolojia inajibu swali hili?

Dunia ipo kwa sababu iliumbwa na Mungu – aliye nafsi binafsi, wa milele, na aliyepo binafsi bila kuumbwa.

(3) Kuna mambo gani matatu yasiyokuwa na mantiki kwa ajili ya dunia?

- Dunia haijatokana na kitu chochote.
- Dunia siku zote imekuwepo kama ilivyo.
- Dunia imetokana na mata au nguvu.

(4) Wasilisha hoja ya Kosmolojia kwa kufasiri vigezo mantiki 2 na hitimisho.

Kigezo mantiki A: Kila kinachoanza kina chanzo.
Kigezo mantiki B: Dunia ilianza.
Hitimisho: Dunia ina chanzo chake.

(5) Ni swali gani linaloulizwa na Hoja ya Teleolojia?

Ni kwa jinsi gani dunia ilipata uratibishaji makini wa muundo wake?

(6) Ni kwa jinsi gani Hoja ya Teleolojia inajibu swali hili?

Muundo tata katika dunia unahitaji Msanifu

(7) Ni swali gani linaloulizwa na Hoja ya Maadili?

Kwa nini wanadamu wana ufahamu wa ndani yao wa kujua mema na mabaya?

(8) Ni kwa jinsi gani Hoja ya Maadili inajibu swali hili?

Ufahamu wa wanadamu wa kujua mema na mabaya unatoka kwa Mungu, Mtoa sheria Mkuu anayetupa sisi maadili.

(9) Wasilisha Hoja ya Maadili kwa kufasiri vigezo mantiki 2 na hitimisho.

Kigezo mantiki A: Ikiwa Mungu hayupo, hakuna misingi ya maadili na uwajibikaji.
Kigezo mantiki B: Misingi ya maadili na uwajibikaji ipo.
Hitimisho: Kwa hiyo Mungu yupo.

(10) Ni upinzani gani ulio wa kawaida sana kuhusiana na uwepo wa Mungu?

Uwepo wa maovu na mateso.

(11) Toa majibu matatu kuhusiana na swali hili, "Inawezekanaje Mungu mzuri na mwenye nguvu zote akawepo kama kuna maovu katika dunia?"

- Maovu ni matokeo ya chaguo la hiari la mwanadamu kutomtii Mungu
- Tatizo la maovu linadhihirisha kwamba Mungu yupo
- Mungu ametoa jibu kwa tatizo la uovu na mateso

(12) Nukuu kutoka kichwani Warumi 1:19-20.

> "Kwa kuwa mambo ya Mungu yanayojulikana yamekuwa dhahiri ndani yao, kwa maana Mungu aliwadhihirishia. Kwa sababu mambo yake yasiyoonekana tangu kuumbwa ulimwengu yanaonekana, na kufahamika kwa kazi zake; yaani, uweza wake wa milele na Uungu wake; hata wasiwe na udhuru."

Somo la 4
Elimu ya Kuitetea Imani ya Uumbaji

(1) Inamaanisha nini kusema kwamba kwa pamoja mageuko na uumbaji ni "maoni yanayotokana imani"?

Siyo mageuko au uumbaji vinavyoweza kuthibitishwa kisayansi kwa sababu hujaribu kuelezea mambo yaliyowahi kutokea nyakati za nyuma.

(2) Sheria ya uhai hutoa uhai inafundisha nini?

Uhai hutoka katika Uhai peke yake

(3) Kwa mujibu wa sheria za **Mwendojoto**, kuna kiasi fulani cha kudumu cha mata na nguvu katika ulimwengu. Nguvu hii inazidi kuendelea kutotumika zaidi na zaidi.

(4) Kwa mujibu wa nadharia ya mageuko, ni masalia gani tunayopaswa tuyatafute?

Maumbo ya mpito ya viumbe kuanzia maumbo rahisi hadi tata kabisa.

(5) Je, Maelezo ya Biblia kuhusiana na uumbaji yanatabiri nini kuhusiana na mabadiliko ya maumbile?

Kutakuwa na Mabadiliko madogo ndani ya aina fulani ya kiumbe. Hakutakuwepo na ushahidi wa mabadiliko ya maumbo ya mpito kutoka aina ya kiumbe mmoja kwenda kwa kiumbe kingine.

(6) Toa mifano mitatu ya ushahidi wa kisayansi kuhusu ulimwengu mchanga.

Yoyote mitatu:

- DNA ndani ya bakteria wa "kale"
- Tishu laini katika mifupa ya *dinosaur*
- Kiwango cha chumvi katika bahari
- Maafa makubwa ya mafuriko ya dunia

(7) Nukuu kutoka kichwani Mwanzo 2:1-3.

"Basi mbingu na nchi zikamalizika, na jeshi lake lote. Na siku ya saba Mungu alimaliza kazi yake yote aliyoifanya; akastarehe siku ya saba, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoifanya. Mungu akaibarikia siku ya saba, akaitakasa kwa sababu katika siku hiyo Mungu alistarehe, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoiumba na kuifanya."

Somo la 5
Hoja za Ujumla kuhusu Imani ya Kikristo

(1) Kuna sehemu ngapi tatu za shauri la Imani ya Kikristo katika somo ili?

- Biblia ni Neno la Mungu.
- Yesu ndiye njia peke yake ya kuingia Mbinguni.
- Imani ya Kikristo ni ya kweli.

(2) Maumbo sita yanayounga mkono shauri la Imani ya Kikristo ni yapi?

1. Agano Jipya inaaminika kihistoria.
2. Unabii
3. Kufufuka
4. Yesu ni Mungu.
5. Yesu hafanyi makosa.
6. Ukristo ni wa kweli.

(3) Orodhesha vigezo mantiki sita na hitimisho lake vinavyoleta shauri la Imani ya Kikristo.

Kigezo mantiki A: Agano Jipya inaaminika kihistoria

Kigezo mantiki B: Yesu alitimiza unabii unaohusiana na Masihi.

Kigezo mantiki C: Yesu alifufuka kutoka kwa wafu.

Kigezo mantiki D: Ufufuko wa Yesu na kutimia kwa unabii kunaonyesha kwamba alikuwa Masihi, Mwana wa Mungu, na Mungu aliyekuja katika hali ya mwili.

Kigezo mantiki E: Kwa kuwa Yesu ni Mungu, hawezi akafanya makosa.

Kigezo mantiki F: Yesu Kristo alifundisha kwamba Biblia ni Neno la Mungu na kwamba peke yake ni njia pekee ya kumwona Mungu.

Hitimisho: Kama Yesu alikuwa Mungu, ni lazima tuamini alichokisema: Biblia ni Neno la Mungu, na Yesu ndiye peke yake njia ya kumwona Mungu. Kwa hiyo, Ukristo ni wa kweli.

(4) Nukuu kutoka kichwani 1 Wathesalonike 2:13.

"Kwa sababu hiyo sisi nasi twamshukuru Mungu bila kukoma, kwa kuwa, mlipopata lile neno la ujumbe la Mungu mlilolisikia kwetu, mlilipokea si kama neno la wanadamu, bali kama neno la Mungu; na ndivyo lilivyo kweli kweli; litendalo kazi pia ndani yenu ninyi mnaoamini."

Somo la 6
Kuaminika kwa Agano Jipya

(1) Jibu pingamizi lifuatalo: "Agano Jipya liliandikwa miaka 100-200 baada ya maisha ya Kristo. Maelezo mengi ya Agano Jipya ni hadithi za kubuniwa." Toa angalao vigezo vitatu vya ushahidi kuunga mkono majibu yako.

Agano Jipya lilikuwa limekamilika ndani ya kipindi cha miaka sitini cha cha kuhesabika maisha ya Yesu.

Ushahidi (zozote tatu):

- Maandishi yamekuwa yakipatikana kuanzia mwanzo wa karne ya pili.
- Mababa wa Kanisa la kwanza kama Clementi na Ignatusi walikuwa wananakili vitabu vya Agano Jipya hadi mwaka 100 B.K.
- Sehemu kubwa ya uandishi wa Agano Jipya utakuwa umefanywa kabla ya Yerusalemu kubomolewa na jeshi la Kirumi mwaka 70 B.K.
- Matendo ya Mitume na nyaraka zote za Paulo ziliandikwa mara tu baada ya kifo cha Paulo katikati ya miaka ya 60.

(2) Kipimo cha Bibliografia kinajaribu kuonyesha nini kinapotumika kwenye nyaraka yeyote ya zamani?

- Inajaribu kutuonesha aidha kama tunayo au hatunayo nakala ambayo ni nakala halisi ya awali.
- Itaonyesha ni kwa usahihi kiasi gani nyaraka imenukuliwa kwa karne zilizopita.

(3) Orodhesha vipengele vitatu vya Kipimo cha Bibliografia vinavyodhihirisha kuaminika kwa Agano Jipya.

- Urefu wa Muda
- Idadi
- Ubora

(4) Watu wengine husema, "Hatuwezi kuamini nakala zetu za Agano Jipya kwa sababu kuna muda mrefu sana kati ya Maandiko ya awali na nakala za mwanzo zilizosalia." Ni kwa jinsi gani kipengele cha *Urefu wa muda* Kipimo cha Bibliografia kinaweza kujibu hiki kipingamizi?

> Urefu wa muda wa Agano Jipya ni mfupi zaidi kuliko kipande chochote kile cha maandiko kutoka ulimwengu wa zamani. Wasomi wanakubaliana na usahihihi wa kuaminika kwa maandishi kwa ajili ya maandiko mengine. Kwa nini isiwe hivyo kwa Agano Jipya?

(5) Toa majibu kwa kipingamizi kifuatacho: "Hata kama kuna muda mfupi kati ya yale maandiko ya asili na zile nakala za mwanzo, kuna tofauti nyingi sana miongoni mwa maandiko yaliyosalia ya Agano Jipya kwa sisi kuweza kujua ni nini kilichokuwemo kwenye maandishi ya asili. Tunazo nakala nyingi sana za maandiko yanayohitilafiana."

> Kiwango kikubwa cha idadi ya maandiko ya Agano Jipya yaliyopo na idadi ndogo ya migongano yake inaonyesha kwamba tunaweza kuliamini Agano Jipya.

(6) Jibu pingamizi lifuatalo: "Hatuwezi kuwaamini waandishi wa Agano Jipya kuweka kumbukumbu sahihi za matukio ambayo yalitokea. Siyo mashuhuda wa kuaminiwa."

> Kipimo cha ushahidi wa ndani na kipimo cha ushahidi wa nje kinaonyesha kwamba Agano Jipya ni kumbukumbu ya historia inayoaminika.

(7) Orodhesha sababu tatu za Agano Jipya kufaulu katika "Kipimo cha Ushahidi wa Ndani."

- Ushuhuda wa kuona kwa macho
- Uwepo wa Mashuhuda walio Hai
- Waandishi waliifia Imani yao

(8) Sheria ya Kutokuhitilafiana ni nini?

> Taarifa haiwezi kuwa ya kweli na wakati huo huo kuwa siyo ya kweli kwa wakati mmoja katika kitu kinachofanana. Kama taarifa moja kabisa inahitilafiana na taarifa nyingine, moja wapo katika taarifa hizo itakuwa siyo ya kweli.

(9) Je, yuko mtu yeyote anayeweza kudhihirisha ukiukwaji halali wa Sheria ya Kutokuhitilafiana katika Maandiko?

> Maandiko hayakiuki Sheria ya Kutohitilafiana.

(10) Orodhesha mistari mitatu ya ushahidi itakayoweza kusaidia Agano Jipya kufaulu kipimo cha Ushahidi wa Nje.

- Ushahidi unaounga mkono kutoka kwa waandishi wengine wa Kikristo wa mwanzo
- Ushahidi unaounga mkono kutoka vianzo vya wasiokuwa Wakristo
- Ushahidi wa uungwaji mkono kutoka elimu ya vitu vya kale

(11) Taja ugunduzi mbili za akiolojia zinazounga mkono usahihi wa historia ya Agano Jipya.

- Kugunduliwa kwa Birika la Bethzatha
- Kugunduliwa kwa Sakafu ya Mawe

(12) Nukuu kutoka kichwani 2 Timotheo 3:16-17.

> "Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema."

Somo la 7 (Mdahalo)
Unabii wa Masihi na Ufufuo

(1) Orodhesha unabii tatu maalumu za Masihi ambazo Yesu alizikamilisha katika maisha yake - kutoka katika jedwali hili.

UNABII ULIOTIMIA KATIKA MAISHA YA YESU	
UNABII	**KUTIMIA**
Kabila la Yuda – Mwanzo 49:10	Luka 3:23, 33
Nyumba ya Daudi – Yeremia 23:5	Luka 3:23, 31
Amezaliwa Bethlehemu - Mika 5:2	Mathayo 2:1
Kutambulishwa na mjumbe – Isaya 40:3	Mathayo 3:1-3
Kufundisha na huduma ya uponyaji – Isaya 61:1, 2; 32:3-4; 35:5	Mathayo 9:24; Luka 4:17-21
Kuishi kabla ya hekalu na Yerusalemu kubomolewa – Danieli 9:26	Hekalu na Yerusalemu vilibomolewa mwaka wa 70 B.K.
Aliitwa Bwana na Mungu – Yeremia 23:6; Isaya 8:6	Luka 2:11; Yohana 29:28
Aliingia Yerusalemu kwa punda – Zekaria 9:9	Mathayo 21:1-8
Kukaa kimya mbela ya washtaki wake – Isaya 53:7	Mathayo 27:12
Kuumizwa kwa maumivu – Isaya 53:5	Mathayo 27:26
Mwili ulichomwa mkuki katika kusulubiwa – Zekaria 12:10	Yohana 19:34
Alizikwa pamoja na matajiri – Isaya 53:9	Mathayo 27:57-60

(2) Kutimia kwa unabii mwingi maalumu za Masihi kunaonesha nini kuhusiana na chanzo cha unabii?

Unabii wote utakuwa umetolewa na Mungu, kwani hakuna mtu yeyote ajuaye mambo ya wakati ujao hata aweze kutabiri mambo mengi kiasi hicho ya wakati ujao kabla hayajatokea.

(3) Orodhesha hoja tatu za wakosoajia wanazozitoa kuhusu kaburi kuwa wazi. Katika kila hoja, toa sababu moja tu kuonyesha kwamba hoja hiyo ina mapungufu.

Maelezo ya 1: Wanafunzi waliuiba mwili wa Yesu.

Sababu hii haitoshi

Sababu yeyote:

- Mitume wasingeweza kuwazidi nguvu walinzi wenye mafunzo wa Kirumi.
- Mitume hawangekubali kuwa tayari kufa kwa taarifa ambayo wangelijua ilikuwa ni ya uongo.

Maelezo ya 2: Mamlaka za Kirumi na Kiyahudi ziliuondoa ule mwili.

Sababu hii haitoshi:

Warumi au Wayahudi wangeweza wakauonyesha mwili kama ulikuwa umefichwa, ili kuweza kuthibitisha kwamba Yesu hakuwahi kufufuka kutoka kwa wafu.

Maelezo ya 3: Yesu hakufa; alikuwa amezirai wakati alipozikwa**.**

Sababu hii haitoshi (Sababu yeyote):

- Askari wa Kirumi walikuwa wamepewa mafunzo ya kuua na kuthibitisha kifo.
- Yesu angekuwa mdhaifu sana kuweza kuondoa lile jiwe na kuwashinda walinzi wa Kirumi

(4) Kuna nini cha muhimu kuhusiana na kumbukumbu ya wanawake waliokuwa miongoni mwa mashahidi wa kwanza kwenye Ufufuko?

Wanawake walikuwa hawana haki ya kisheria kusimama katika ulimwengu wa kale. Kama waandishi wa vitabu vya Injili wangekuwa wanatunga taarifa hii, wangetumia mashuhuda wa kiume.

(5) Kuna nini cha muhimu kuhusu ibada ya kuabudu ya Wakristo wa mwanzo wakiabudu katika kila siku ya kwanza ya wiki na kusherehekea Pasaka kila mwaka?

Wakristo wa kwanza waliamini katika hali ya uhalisia wa mwili kufufuka. Ushahidi wa macho unathamanishwa na wanahistoria.

(6) Nukuu kutoka kichwani 1 Wakorintho 15:3-6.

> "Kwa maana naliwatolea ninyi hapo mwanzo yale niliyoyapokea mimi mwenyewe, ya kuwa Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo maandiko; na ya kuwa alizikwa; na ya kuwa alifufuka siku ya tatu, kama yanenavyo maandiko; na ya kuwa alimtokea Kefa; tena na wale Thenashara; baadaye aliwatokea ndugu zaidi ya mia tano pamoja; katika hao wengi wanaishi hata sasa, ila baadhi yao wamelala."

Somo la 8
Madai ya Yesu kuwa Yeye ni Mungu

(1) Orodhesha kauli nne za wakati wa huduma yake kuonyesha kwamba Yesu alijiamini kwamba ni Mungu.

- Yesu alisema kuwa yeye ni "MIMI NIKO" wa Agano la Kale.
- Yesu alisema yeye ni mmoja pamoja na Mungu Baba.
- Yesu alisema anazo sifa za Kimungu.
- Yesu alisema kuwa anao uweza wa kutenda mambo ya kiungu.

(2) Orodhesha kauli tatu za wakati wa kuendelea kwa kesi yake kuonyesha kwamba Yesu alijiamini kwamba ni Mungu.

- Yesu alidai kuwa ni Masihi.
- Yesu alidai kuwa Mwana wa Mungu.
- Yesu alidai kuwa Mwana wa Mtu.

(3) Je, ni chaguzi ngapi tano za kuzingatia kwenye madai ya Yesu ya kujinasibu kwamba yeye ni Mungu?

- Je! Yesu alikuwa ni Hadithi?
- Je! Yesu alikuwa ni Guru?
- Je! Yesu alikuwa ni Mwongo?
- Je! Yesu alikuwa ni Kichaa (Mtu punguani)?
- Je! Yesu alikuwa ni Bwana?

(4) Kwa kifupi elezea tatizo la kila kipengele katika chaguzi nne za mwanzo.

Hadithi: Agano Jipya kihistoria linaaminika.

Guru: Yesu alikuwa ni Myahudi aliyekuzwa kikamilifu kabisa katika utamaduni wa Mungu mmoja. Hakuna Myahudi atakayetokea kusema kwamba sisi wote ni miungu.

Mwongo: Yesu hangeweza kuwa mwongo kwa sababu ya tabia yake, kwa sababu hakuwa na sababu ya kumfanya aseme uongo, na kwa sababu ya Kufufuka.

Punguani: Yesu alikuwa mkamilifu katika ujumla wa nafsi yake.

(5) Andika Kauli sita na hitimisho kwa ajili ya hoja ya Ujumla ya Ukristo.

Kigezo mantiki A: Agano Jipya inaaminika kihistoria

Kigezo mantiki B: Yesu alitimiza unabii unaohusiana na Masihi.

Kigezo mantiki C: Yesu alifufuka kutoka kwa wafu.

Kigezo mantiki D: Ufufuko wa Yesu na kutimia kwa unabii kunaonyesha kwamba alikuwa Masihi, Mwana wa Mungu, na Mungu aliyekuja katika hali ya mwili.

Kigezo mantiki E: Kwa kuwa Yesu ni Mungu, hawezi akafanya makosa.

Kigezo mantiki F: Yesu Kristo alifundisha kwamba Biblia ni Neno la Mungu na kwamba peke yake ni njia pekee ya kumwona Mungu.

Hitimisho: Kama Yesu alikuwa Mungu, ni lazima tuamini alichokisema: Biblia ni Neno la Mungu, na Yesu ndiye peke yake njia ya kumwona Mungu. Kwa hiyo, Ukristo ni wa kweli.

(6) Nukuu kutoka kichwani Yohana 20:30-31.

"Basi kuna ishara nyingine nyingi alizozifanya Yesu mbele ya wanafunzi wake, zisizoandikwa katika kitabu hiki. Lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake."

Somo la 9
Upekee wa Ukristo katika Dini Nyingi

(1) Orodhesha imani tano kubwa zinazohusiana na uwepo na asili ya Mungu. Fafanua kila moja.

Imani kwamba hakuna Mungu: Inafundisha kwamba hakuna Mungu.

Imani kuwa Mungu yumo ndani ya kila kitu na kuwa kila kitu ni Mungu: Inafundisha kwamba kuna uwezo wa mungu, lakini huyu mungu hana tofauti na ulimwengu.

Imani kuwa Mungu anautegema ulimwengu aweze kuwepo: Inafundisha kwamba Mungu ni tofauti na ulimwengu lakini anautegemea ulimwengu ili aweze kuwepo.

Imani ya kuabudu miungu wengi: Inafundisha kwamba kuna miungu wengi.

Imani ya kumwamini Mungu mmoja tu: Inafundisha kwamba kuna Mungu mmoja tu aliye tofauti na dunia, wa milele, binafsi na aliye na uweza wa kiungu.

(2) Kuna tofauti gani kati ya Ukristo na imani nyingine kubwa?

Ni Ukristo peke yake unaoonesha njia kwa ajili ya mwanadamu kusamehewa dhambi zake na kupatanishwa na Mungu, na peke yake ulioonesha njia ya kumrejesha mwanadamu kwenye sura na mfano wa Mungu.

(3) Kuna vigezo mantiki gani vitatu na hitimisho ambavyo vinaonyesha ushahidi wa kibiblia wa imani ya Utatu Mtakatifu?

Kigezo mantiki A: Kuna Mungu mmoja tu.

Kigezo mantiki B: Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu wanatambuliwa na Maandiko kama Mungu.

Kigezo mantiki C: Hizi Nafsi tatu yanahusiana zenyewe na kwa dunia kama Nafsi tofauti.

Hitimisho: Mungu mmoja wa kweli wa Biblia alijidhihirisha mwenyewe kuwepo katika Nafsi tatu tofauti: Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Mungu ni mmoja kwa asili, lakini katika Nafsi tatu.

(4) Ni mambo gani matatu ya ulimwengu yanaonyesha imani ya Utatu Mtakatifu?

- Nafasi
- Muda
- Mata

(5) Fafanua *Imani katika mizimu.* Ni nini tofauti kubwa iliyopo kati ya Imani katika mizimu na Ukristo?

Imani katika mizimu ni mtazamo katika nguvu za asili na roho za mababu (mizimu) kuwa ni vitu hai vyenye utambulisho tofauti.

Labda tofauti kubwa iliyoko kati ya Imani katika mizimu na Ukristo ni uhusiano uliopo kati ya Mungu na mwanadamu.

(6) Fafanua *Usawazishaji*. Kwa nini usawazishaji haukubaliki kwa Wakristo?

Usawazishaji ni uchanganywaji wa Ukristo wa kweli na dini nyingine.

Haukubaliki kwa sababu Biblia inafundisha kwamba kuna njia moja peke yake ya kumwendea Mungu.

(7) Imani ya Neema iliyotangulia ni nini?

Ni neema inayotangulia kabla ya kukombolewa. Neema iliyotangulia ni kwa ulimwengu wote, lakini pia inaweza ikakubalika au ikakataliwa.

(8) Nukuu kutoka kichwani Matendo 4:11-12.

"Yeye ndiye jiwe lile lililodharauliwa na ninyi waashi, nalo limewekwa kuwa jiwe kuu la pembeni. Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo."

Kristo-katikati. Mafunzo. Kila Mahali.

SHEPHERDSGLOBAL.ORG